**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAHIMBA
S.L.P 443, BUHIGWE,
KIGOMA.
TAREHE 15.11.2025

SIMU: 0757470345- MKUU WA SHULE
0766742841- MAKAMU WA SHULE
0740324539- MTAALUMA
0742429043- MWALIMU MLEZI

Kumb. Na KHGSS/A1/J1/01/2025.

JINA LA MWANAFUNZI ____________________________________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAHIMBA KIDATO CHA KWANZA, HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE.**

**1.0.UTANGULIZI.**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2025, Hongera sana. Shule ni ya bweni ya wasichana. Muhula wa kwanza utaanza tarehe 13.01.2026 hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 12.01.2026 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17.01.2026

Shule ipo katika kijiji cha KASUMO umbali wa kilometa 30 kwa magari yatokayo Kasulu. Nauli ni Tsh 7000.

Kwa wale watokao wilaya nyingine, fika Kasulu mjini katika stand ya Bogwe, panda magari yanayofika katika Kijiji cha **MUYAMA**, mwambie dereva kuwa unahitaji kufika katika **SHULE YA SEKONDARI YA**

WASICHANA KAHIMBA.

## 2.0. MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 1.SARE ZA SHULE

MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NA SARE SAHIHI KAMA INAVYOONEKANA KATIKA PICHA. ILI KUEPUKA MAKOSA KATIKA RANGI HUTAKIWI KUPRINTI PICHA HIZI, UNASHAURIWA KUPAKUA(DOWNLOAD) PICHA HIZO. KAMA UNAHITAJI MAELEZO ZAIDI KUHUSU SARE, TAFADHALI PIGA SIMU KUPATA MAELEZO SAHIHI.

(i) Sketi mbili mshono rangi na urefu iwe kama inavyoonekana katika picha. Kitambaa kiwe kizito.



(ii) Tai mbili ifikie kwenye mkanda wa sketi kama inavyoonekana katika picha.

(iii) 

(iv) Shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi

(iii)Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (02)

(iv)Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

(v) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na kisigino kirefu (yeboyebo hazitakiwi), kiwi nyeusi, na brush ya viatu.

(vi) T-shirt mbili (02) nzito rangi ya bluu bahari, zenye kola kama invyoonekana katika picha hapo chini. Tshirt zitawekwa nembo ya shule baada ya mwanafunzi kuripoti shule.

(vii) 

(viii) Sweta rangi ya damu ya mzee yenye V.

(ix) Vazi la hijabu linatakiwa kuwa lenye kitambaa kizito (cheupe) kisichoonesha maumbile na iwe ndefu kupita kifua. Pia mtoto ashonewe hijab rangi ya kijivu atakayovaa wakati wa kazi.Hijabu nyeupe itavaliwa muda wa masomo tu.

(x) Aje na taulo la kuogea na sio kanga.

(xi) Track suit jozi mbili rangi ya bluu bahari yenye mistari meupe.

(xii) Shamba dress mbili (gauni la kuvaa wakati wa kazi za nje) kitambaa kizito rangi ya damu ya mzee mshono wa solo mikono iwe ya size ya shati la mikono mifupi.

(xiii) Aje na tranka (begi la chuma) la kuwekea vitu vyake.

(xiv) Aje na net ya mbu.

## 2.1.VIFAA VYA TAALUMA

Kila mwanafunzi anashauriwa kuwa na vifaa vya taaluma vifuatavyo:-

(i) Aje na vitabu kwa kila somo kwa ajili ya

kujisomea.

ii) Daftari kubwa kumi (10) kaunta books quire three.

iii) Mkebe wa Hisabati. (Mathematical Instrument set)

iv) Kamusi ya kingereza kwa kingereza.

(iv) Koti ya **maabara (laboratory Coat) yenye rangi nyeupe mikono mirefu,urefu kupita magoti ni muhimu.**

(v) **Mathematical Table ya baraza** la mitihani.

(vii) Aje na **Rimu mbili** za karatasi.

(viii) Aje na fedha ya kununua pazia

(ix) Rula

(x) Begi la kubebea madaftari.

(xi) Aje na taa /tochi ya kumulika pale umeme unapokuwa umekatika.

Vifaa hivi ni kwa ajili ya matumizi binafsi ya Mwanafunzi.

## 2.3. MAHITAJI MENGINE YA KIBINADAMU

Kwa ajili ya usafi binafsi na mazingira hakikisha unakuja na vitu vifuatavyo:

-

(a) Aje na ufagio wenye mpini mrefu (wa kusimama) kwa ajili ya kufagia nje.

(b) Godoro la sponji ($2^1/_2$ nchi)

(c) Shuka mbili za rangi ya pink, Blanketi, mto, taulo, na chandarua.

(d) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.

(e) Vyombo vya chakula (kijiko, sahani, bakuli, na kikombe)-visiwe vya plastiki

(f) Kwanja moja (01),Mopa moja (01), na Jembe moja (01) na mpini wake.

(g) Hard broom 1.

(h) Soft broom 1.

(i) Chombo cha kuhifadhia maji safi ya kunywa (dumu la lita 5)

(j) Aje na vifaa vya usafi binafsi kama vile mswaki, dawa ya meno, mafuta, sabuni za kufulia na kuogea.

(k) Aje na kandambili za kuogea.

(l) Aje na tochi ndogo imara na betri zake ( itatumika iwapo umeme umekatika

(m) )Aje na passport size tatu (03) ipigwe akiwa amevaa shati jeupe)

(n)Aje na sanduku la chuma au bati lisiwe begi pamoja na kufuli.

o) Aje na blueband kilo moja yenye Omega 3 kwa ajili ya kuweka kwenye uji ili kuboresha uwezo wa uelewa na kumbukumbu katika masomo yake.

## 3.0. **SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu, Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo kwa umakini mkubwa sana.

(i) Mahudhurio katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima **(UTORO HAPA KWETU NI MWIKO**).
(ii) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunziwengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(iii) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(iv) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule.
(v) Kuvaa Sare ya Shule wakati wote unapotakiwa.
(vi) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote unapotakiwa.
(vii) Kutunza mali za umma.

## 3.1. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi.
2. Kumiliki/ kutumia **SIMU** katika mazingira ya shule bila ruhusa.
3. Uasherati, ushoga na ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
5. Kupiga au kupigana.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Utoro wa aina yoyote pamoja na kutokuhudhuria masomo bila sababu.
8. Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
9. Kuwa na mimba
10. Kuoa au kuolewa
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kungoza au kushiriki kuvuruga amani.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kuwa na simu ya mkononi(mwanafunzi atatumia simu ya shule)

AHADI ZA SHULE

**AHADI NA UTII WA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.**

Mimi ____________________________________________________

Naahidi kwamba nitafuata na kutii kwa muda wote nitakaokuwa ninasoma hapa shuleni.kanuni na sheria zifuatazo za Shule hii.

Sahii______________ Tarehe ___________

**NI MARUFUKU:**

1. Kuanzisha/ kushiriki kwenye migomo, fujo au ukaidi wa aina yoyote, daima nitatumia taratibu halali ili kutafuta ufumbuzi wa matatizo yatakayojitokeza.
2. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, picha za viongozi wa Serikali na Bendera ya Taifa.
3. Kuiba
4. Kuwa mwasherati/kujihusisha na mapenzi shuleni.
5. Kutumia kilevi na pombe ya aina yoyote.
6. Kuvuta sigara au bangi.
7. Kupata au kutoa mimba.
8. Kupigana .
9. Kutoroka au **kutokuhudhuria** darasani bila taarifa maalum
10. Kwenda nje ya Shule bila Sare au Ruksa ya Mwalimu wa yeyote yule.
11. Kuoa au kuolewa
12. Kuwa mvivu.
13. Kupatikana na makosa ya jinai

**Endapo nitavunja Sheria mojawapo kati ya hizo nitakuwa tayari kupokea adhabu moja wapo au zaidi kati ya zifuatazo:-**

(a)Kuchapwa viboko (visivyozidi **vinne** kwa kila kosa )
Mikononi ( Wasichana) kwa kunyoosha mkono bila kukwepa.

(b) Kufanya kazi ngumu kama vile, kutengeneza barabara, kuchimba shimo la takataka, kufyeka nyasi/ vichaka, kuokota mawe,kulima n.k (c)Kupewa onyo kali kimaandishi.

(d) Kusimashwa shule kwa muda wa siku 21 za masomo.

(e) Kufukuzwa shule na Bodi ya shule.

**MWISHO:**
Gharama zote za kwenda nyumbani na kurudi Shuleni ni juu ya Mzazi/ Mlezi

____________________ ____________________

Sahihi ya Mwanafunzi Sahihi ya Mzazi/Mlezi
Tarehe: __________________ Tarehe: ______________
Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi__________________________________________

**UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI; -**
Nathibitisa kuwa maelezo niliyoandika katika fomu hii ni sahihi.
Jina ______________________________________________________________
Sahihi ______________________________________________________________
Tarehe ______________________________________________________________

## 4.0.MAAGIZO MENGINE

### (i) FEDHA YA MATUMIZI

Mzazi ahakikishe anamnunulia binti wake mahitaji muhimu, pia ampe fedha ya kutosha kwa ajili ya mahitaji madogo madogo ambayo hupatikana katika duka lililopo eneo la shuleni.

### (ii) MATIBABU YA MTOTO

Gharama zote za matibabu zitagharimiwa na mzazi/mlezi. Hivyo mzazi mkatie bima ya afya mwanao. Kama hana bima ya afya lipia TSH 50,400 katika account ya shule ili mwanao aweze atengenezewe bima ya afya (NHIF). **JINA LA AKAUNT: KAHIMBA SECONDARY SCHOOL CAP. NMB ACCOUNT NUMBER 53310001070**

**ANGALIZO:**

**BIMA YA AFYA NI LAZIMA. HATUTAMPOKEA MTOTO AMBAYE HANA BIMA YA AFYA.**

### . (iii)VYETI BANDIA VYA HOSPITALI

Baadhi ya wazazi hushirikiana na watoto wao kutafuta taarifa bandia ili wasifanye kazi za shule au kula vyakula aina Fulani. Mzazi au mtoto asifanye hivyo kwa kuwa mazingira hayatamfaa kujifunza.

Ni kosa kwa mwanfunzi kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa. Ruhusa ya kutoka nje ya eneo la shule ni lazima ipatikane kutoka kwa mwalimu wa zamu ambaye atatoa karatasi maalumu ya ruhusa. Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na makamu mkuu wa shule baada ya kupelekwa maombi kwa kupitia kwa mlezi wa nyumba na mwalimu wa zamu anayehusika. Mwanafunzi

aliyeruhusiwa kwenda nje ya mipaka ya shule lazima avae sare ya shule.

Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:-

(i)Ofisi ya walimu
(ii)Ofisi za shule
(iii)Nyumba za watumishi wote wa shule
(iv)Karakana.

•Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-

(i)Vilabu vya pombe
(ii)Nyumba za starehe kama dansi,filamu au video n.k
(iii)Nyumba za kulala wageni.

2.**UTARATIBU WA MABWENI**.

(i) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa bwenini wakati wa vipindi madarasani, vipindi vya kujisomea (usiku) na shughuli nyingine za kishule nje ya madarasa isipokuwa kwa ruhusa maalum.
(ii) Bweni lazima lisafishwe kila siku asubuhi na wanfunzi wote lazima watandike vizuri vitanda vyao kabla ya kwenda darasani.
(iii)Mgeni yeyote haruhusiwi kuingia kwenye mabweni ya wanafunzi.
(iv) Radio zote na vyombo vya muziki,mabwenini vifungwe baada ya kuzima taa na wanafunzi wote lazima wawe kimya wamelala.
(v) Ni marufuku kubandika picha kwenye kuta za mabweni, madarasa na sehemu nyingine zizungukazo mazingira ya shule hii na sehemu nyingine nje ya shule.

Mimi______________________________________________(mzazi/mlezi)
Wa______________________________________________(Jina kamili)nimeelewa na kuzingatia taratibu zote hapo juu.
Sahihi__________________________ Terehe_________________________

3.**SHERIA ZA MADARASANI**.

(i) Lazima kuwahi darasani na kuukaa kimya mda wote.
(ii) Hairuhusiwi kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyemo darasani.
(iii) Akitaka kuuliza swali au kujibu swali mwanafunzi anyooshe mkono na kusimama baada ya kuruhusiwa kufanya hivyo.
(iv) Kila mwanfunzi ahudhurie vipindi vyote.
(v) Kila mwanafunzi atunze usafi wa darasa lake.

**4.MBAO ZA MATANGAZO.**

(i) Ni marufuku mwanafunzi kuondoa au kuweka tangazo lolote katika mbao zozote za matangazo shuleni bila ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu.

**5.UPOKEAJI WA WAGENI**

(i) Wazazi/walezi watatembelea watoto wao jumamosi ya mwisho wa mwezi tu.

(ii) Wageni wote wa wanafunzi waripoti kwenye ofisi ya makarani/mwalimu wa zamu na mwanafunzi anayehusika ataitwa aonane nae.

(iii) Mzazi haruhusiwi kumletea chakula cha aina yoyote.

**6.BARUA ZA WANAFUNZI.**

(i) Barua zote za kiofisi za wanafunzi lazima zipitie kwa mkuu wa shule.

(ii) Mhudumu wa ofisi atakuwa na madaraka ya kuchukua barua, vifurushi na hati zote za kifedha kutoka kwa wahusika ambao itabidi waonyeshe vitambulisho na kutia sahihi kuwa wamepokea.

**7.MAGONJWA**

(i) Mwanafunzi akiugua atoe taarifa haraka kwa mwalimu wa afya ili asaidiwe. Wanafunzi wenye maradhi ya muda mrefu kama pumu ama allergy watoe taarifa mara wafikapo shuleni.

5. 0. **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOTAKIWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

(a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya serikali (HAKIKISHA MWANAO ANAPIMA KIKAMILIFU) Fomu hii iwasilishwe kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo,utoro, na makosa ya jinai. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

6.0. **TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO NA KUYATEKELEZA KKIKAMILIFU.**

**7.0. KAULI MBIU YA SHULE, "SCHOOL MOTTO "EDUCATING GIRLS FOR A BRIGHTER TOMMOROW".**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

FARAJA TIMOTHY LWIMBO
MKUU WA SHULE
0757470345

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAHIMBA

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

To medical officer I/C of ______________________________District/region/Referal Designated Hospital,P.O.BoX_______________________________________________

Please examine the above named in full as to this physical and fitness for being to pursue four years of secondary school education. In case of an acute or defect/disability in each category, or sub category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to school of students with special needs.

(To be completed by a Medical officer in respect of all form Entrants)

Student's full name ________________________________________________________

Age ____________(**Year**) ___________Sex __________________________

Blood count (**Red and White**) ____________________Stool examination ___

Urinalysis ______________________________________________________________

Syphilis andother__________________________________________________________

Venereal disease test_________________________________________________

T.BTest __________________________________________________________

EyeTest __________________________________________________________

Ears Chest _______________________________________________________

Spleen __________________________________________________________________

Abdomen ______________________________________________________________

Urine test for pregnancy_______________________________________________

Additional information eg. Physical defect or impairment(**s**), chronic infections or family diseases _______________________________________________________________

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signed ____________________

Designation ____________________

Station ____________________

Date: ____________________

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

KAHIMBA GIRLS SECONDARY SCHOOL

HISTORIA YA MWANAFUNZI

Bandika picha ya rangi ya mwanafunzi awe na shati jeupe

1. Jina la mwanafunzi ____________________ Dini /Dhehebu ____________________
2. Jina kamili la Baba ____________________
3. Je Baba yuko hai au amefariki ____________________
4. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki ____________________
5. Jina kamili la Mama ____________________
6. Je mama yuko hai au amefariki ____________________
7. Kama amefariki taja tarehe au mwaka aliofariki ____________________
8. Anuani ya Mzazi ____________________
   Jina la kijiji /Mji____________________
   S.L.P____________________
9. Kazi aifanyayo Baba ____________________
10. Sehemu anayofanyia kazi ____________________
11. Kazi aifanyayo Mama ____________________
12. Sehemu anakofanyia kazi____________________
13. Kama huishi na Mzazi wako taja jina la Mlezi wako ____________________
14. Kazi aifanyayo____________________
15. Sehemu anakofanyia kazi ____________________
16. Anuani ya Mlezi ____________________

Jina la kijiji /Mji________________________________________

**S.L.P**____________________________________________

17. Habari nyingine za familia ;

Jina la Kaka / Dada __________________________________________

Umri________kazi yake ____________________ Mahali anapofanyia kazi

______________________________________________________

18. Afya ya Mwanafunzi (Tafadhali eleza kama una ugonjwa wowote ambao una kukabili kwa hiyo unastahili huduma muhimu) Ni muhimu umfahamishe Daktari atakaye kupima ili naye aweze kujaza katika sehemu inayomuhusu kwenye fomu kwa ushauri zaidi wa kitaalamu.

______________________________________________________________

______________________________________________________________

___________________________________________